UK 21

Sh. milioni 200>> Fedha zilizotengwa kununulia vifaa na

# Serikali yaja na mikakati kuinua sekta ya uvuvi

Na MWANDISHI WETU, *Dodoma*

SERIKALI imesema imedhamiria kuendeleza sekta ya uvuvi nchini kwa kuhakikisha inanunua zana bora za uvuvi za wavuvi ili shughuli za uvuvi ziwe endelevu na kukuza kipato cha nchi.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki katika ofisi za wizara hiyo zilizopo Mtumba Jijini Dodoma, wakati wa hafla ya kukabidhi injini sita za kupachika katika boti kwa vyama sita vya ushirika wa wavuvi.

Alibainisha kwamba nia ya serikali ni kuona mchango wa pato la taifa katika sekta ya uvuvi unakua kwa kujenga mazingira mazuri ya kuvua rasilimali za uvuvi zilizopo nchini.

"Kwa mwaka jana na mwaka huu serikali imetenga sh. milioni 200 kununua vifaa na zana mbalimbali za uvuvi kwa ajili ya wavuvi," alisema.

Ndaki aliweka bayana kwamba injini hizo zenye thamani ya sh. milioni 58.7 zilizotolewa kwa vyama vya Kabwe kilichopo Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, Mwamgongo (Kigoma Vijijini - Kigoma), Msanga Mkuu (Mtwara Vijijini - Mtwara, Kilwa Kivinje (Kilwa –Lindi) Igombe (Ilemela - Mwanza) na Chembaya (Bushosa –Mwanza), ni sehemu ya fedha iliyoidhinishwa na serikali kwa ajili kuwasaidia wavuvi.

Katika kuhakikisha wavuvi wanaendelea kupata misaada mbalimbali kutoka serikalini, aliwasihi wajiunge na vyama vya ushirika wa wavuvi vinavyotambulika kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa na taifa na kazi zao ziwe zinafanyika kwa kufuata utaratibu unaoeleweka.

Aidha, aliwataka wavuvi kuelimisha na kutoendeleza uvuvi haramu kwa kuwa hauna tija, husababisha madhara kwa mazalia ya samaki na kuharibu shughuli za uvuvi endelevu.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Abdallah Ulega, alitoa rai kwa wadau wa sekta ya uvuvi nchini kuwa, hatua ya kukabidhi injini hizo za kupachika iwe chachu ya kujipanga vyema kwa kuwa fursa zipo nyingi katika sekta hiyo.

Ulega aliwataka wadau hao kuhakikisha vyama vyao vya ushirika wa wavuvi vinakuwa imara na vifanye kazi kwa kufuata utaratibu na kwamba serikali imejipanga kuhakikisha wavuvi wanainuka na kuchangia zaidi katika pato la taifa kupitia sekta ya uvuvi nchini.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, alisema wizara imekuwa ikitoa injini hizo mara kwa mara kwa vyama vya ushirika wa wavuvi ambavyo vimesajiliwa na kutambuliwa kisheria pindi inapopata fedha.

Pia, alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikitumia vigezo mbalimbali kwa vyama vya ushrika vya wavuvi kupata injini za boti, kikiwemo cha ushirika wao katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi na kufafanua kuwa vyama hivyo sita vimekidhi kigezo hicho kwa kuwa wamekuwa wakishirikiana na wizara katika kupiga vita uvuvi haramu.

Akizungumza kwa niaba ya wabunge kutoka majimbo yaliyotoa vyama sita vya ushirika wa wavuvi, vilivyokabidhiwa injini za kupachika katika boti, Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Dk. Angeline Mabula ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alitaka kuwepo kwa elimu zaidi kwa kulinda maeneo yanye mazalia ya samaki na kuwepo uvuaji wa samaki kwa vipindi.

Dk. Angeline alisema kwa sasa wavuvi wameelewa kuhusu uvuvi haramu, hivyo ni vema kulinda na kusimamia maeneo ya mazalia ya samaki kutovamiwa na wavuvi na kuharibu uendelevu wa uvuvi katika maeneo yao.

UZINDUZI

Goes National

Scanned with CamScanner

Meneja Msimamizi wa Taasisi ya Elimu ya WIPAHS, Jabbir Rajan (katikati), akigonganisha mikono na wakurugenzi wa kampuni ya kutengeneza na kuunganisha magari ya GF Assembing, Imran Karmal (kulia) na Ali Jawad (kushoto), baada ya kupokea msaada wa vitanda, meza na viti vya kusomea vilivyotolewa na kampuni hiyo, kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum wanaosoma katika shule za tasisi hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

SEPT 15, 2021 NIPASHE UK 9

# Mamlaka kuja kufuatilia masoko mazao ya mifugo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ametangaza kwamba serikali itaunda mamlaka itakayoratibu na kusimamia malisho ya mifugo na kuyatafutia masoko mazao yanayotokana na sekta ya mifugo. Ndaki alibainisha hayo kwenye mkutano wa wadau wa mifugo uliomalizika jana jijini Dar es Salaam, na kwamba serikali inajali maslahi ya wafugaji na kwamba itatekeleza mawazo ya wadau wa sekta ya mifugo katika kuboresha sekta hiyo na kutengeneza mazingira bora ya ufugaji, lengo iendelee kutoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya Taifa.

Waziri Ndaki amesema serikali inafikiria kuanzisha mamlaka itakayosimamia malisho na masoko ya mifugo na mazao yake na kubainisha kuwa mamlaka hiyo itafanya bidii kuinua sekta hiyo pamoja, kupunguza migogoro na kuhamahama kwa wafugaji.

"Serikali itaunda mamlaka hii na moja ya jukumu lake kubwa ni kuaangazia malisho na kutafuta masoko ya mazao ya sekta hii ya mifugo," ameeleza Waziri Ndaki.

Amesema aliutumia mkutano huo kuwatia moyo na kuwahakikishia wafugaji kwamba serikali ipo na itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wafugaji kwa kuwa inatambua mchango wao katika maendeleo uchumi wa taifa pamoja na kutengeneza ajira kwa vijana.

Kaimu Mkurugenzi wa Mipango na Utafiti wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Mzee Kilele, ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Frank Nyabundege, aliwahakikishia wadau wa sekta ya ufugaji ushirikianao kutoka TADB, na kwamba mikutano yenye malengo mazuri kama huo, inaipa benki yao fursa ya kujua, kutambua na kuona jinsi gani inaweza kuwafikia wafugaji wengi zaidi ili waweze kunufaika na fursa zitolewazo na benki hiyo. "Hii imekuwa fursa nzuri kwetu kuwapo hapa. Mkutano huu unatoa nafasi kwetu kukutana na wadau wa sekta ya mifugo na nachukua fursa hii kuwahikikishia kuwa benki itaendelea kuongeza kasi katika kutoa mikopo pamoja na kuongeza thamani ya mazao ya mifugo ili kuifanya kuwa sekta imara yenye kuleta tija kwa wafugaji wenyewe na katika kuinua uchumi wa taifa," alisema Kilele.

Alieleza kuwa hadi Agosti mwaka huu, benki hiyo imetoa mikopo ya moja kwa moja kwenye sekta ya mifugo yenye thamani ya Sh. bilioni 23.8 na fedha hiyo imewezesha AMCOs 5 kupata ng`ombe wa kisasa na kunufaisha wafugaji 128. Aidha, Kilele alisema benki imetoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 11.8 na fedha hiyo imewezesha ujenzi wa viwanda vinne vya maziwa.


"Kwa kutambua umuhimu wa sekta hii na uhusiano mkubwa wa kati ya sekta ya mifugo na maziwa tuliona ni vyema tutoe mikopo ambayo iliwezesha ujenzi wa viwanda vinne vya maziwa na wafugaji zaidi ya 6,000 wanauza maziwa yao kwenye viwanda hivyo," alieleza Kilele.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wafugaji Wilaya ya Karagwe mkoani Kagera, Jackson Kamkoto, alisema ukosefu wa elimu kwa wafugaji, uhaba wa maofisa ugani, uhaba wa malisho na maji zimekuwa changamoto kubwa zinazowakabili wafugaji na kupendekeza serikali kuunda chombo maalamu kitakachoratibu masuala hayo ili kuongeza tija kwenye sekta ya ufugaji.

Scanned with CamScanner

# HABARI MBEYA





Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kushoto), akisaidiana na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Kituo cha Uyole jijini humo, Dk. Edwin Chang'a, kubeba mkate wa malisho aina ya hey unaozalishwa na kituo hicho kwa ajili ya kukabiliana na matatizo ya uhaba wa malisho kwa wafugaji hasa kipindi hiki cha kiangazi alipowatembelea hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

Scanned with CamScanner

THE GUARDIAN Page 7.



Mbeya regional commissioner Juma Homera (L) and the director of the Tanzania Livestock Research Institute's Uyole centre, Dr Edwin Chang'a, pictured at the weekend checking hay prepared as stock for use by herders when natural pasture gets scarce. Photo: Correspondent Nebart Msokwa